



JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAISI
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSOKELO



TANGAZO TANGAZO TANGAZO

**TANGAZO LA ZABUNI YA UKODISHAJI NA UENDESHAJI WA
MAGHALA YA MAZAO**

05.06.2024

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo anawatangazia wananchi, Makampuni na watu binafsi kuwa anakaribisha maombi ya zabuni kwa ajili ya ukodishaji na uendeshaji wa maghala ya kuhifadhia zao la kokoa.

Maghala yanayokodishwa kwa ajili ya uendeshaji ni kama ifuatavyo.

1. Ghala lililopo kata ya Kisegeze Zabuni Namba LGA/BDC/157/2023/2024/NC/07.
2. Ghala lililopo kata ya Ntaba Zabuni Namba LGA/BDC/157/2023/2024/NC/08.

Waombaji wanatakiwa kutimiza Sifa/Vigezo vifuatavyo-;

1. Awe ni raia wa Tanzania na kama ni kampuni iwe na usajili wa Tanzania
2. Awe na Uzoefu wa uendeshaji wa Ghala
3. Awe na vifaa muhimu vya kupimia mazao kama Mizani za Kisasa, Vipimo vya ubora wa Mzao na Vipimo vya unyevu.
4. Awasilishe taarifa za kifedha za miezi sita kuanzia tarehe 01.12.2023 hadi tarehe 30.05.2024
5. Awe na uwezo wa kulipia ghala kama makubaliano yatakavyofikiwa.
6. Maombi yataje kiasi atakacholipa kwa kila kilo itakayohifadhiwa kwenye ghala.
7. Kabrasha la Maombi ya Zabuni linapatikana ofisi ya Manunuzi na Ugavi baada ya kulipa ada ya zabuni kiasi cha Tsh. 100,000 kwa kila Zabuni/Ghala atakayoomba, kiasi hichi cha malipo hakitorejeshwa.

8. Kila ghala/Zabuni itaombwa Peke yake.
9. Maombi yafungwe kwenye bahasha kwa lakiri na kuandikwa namba ya Zabuni na kuwasilishwa kwa Katibu wa Bodi ya Zabuni Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo S.L.P 2, Tukuyu.
10. Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 18.06.2024 Siku ya Jumanne saa 10:30 za asubuhi na ufunguzi wa zabuni utafanyika tarehe 18.06.2024 saa 10:30 za asubuhi katika ukumbi wa Halmashauri Makao Makuu.



Chrispin Mnganya

**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA
HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSOKELO**

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)
BUSOKELO**